

Hii ni shule ya Msingi
Msewe

Kupitia Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho lilikabidhi rasmi **Mradi** wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika Shule ya Msingi Msewe (iliyopo Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam) yenye thamani ya shilingi milioni 889.

Ilikuwa ni

JULAI 15, 2025



Miundombinu iliyokabidhiwa

Kupitia ufadhili huo wa shilingi milioni 889, kanisa lilikamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ifuatayo

- Madarasa mapya 16, yamejengwa ili kupunguza msongamano wa wanafunzi.
- Madarasa Manne (4) chakavu yaliyokuwepo shuleni hapo yalifanyiwa ukarabati.
- Jengo la utawala, limejengwa kwa ajili ya ofisi za walimu na uongozi wa shule.
- Matundu ya vyoo 12 yamejengwa ili kuboresha hali ya usafi na mazingira ya kujifunzia, na;
- Mfumo wa maji umehusisha ujenzi wa stendi na ufungaji wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 15,000



Jengo la Utawala



Darasa lililokarabatiwa



Nyaigesha atunukiwa cheti

Katika hafla hiyo, Diwani wa Kata ya Msewe Mh. Jafar Juma Nyaigesha alipongezwa na kutunukiwa cheti kwa kutambua mchango wake na jitihada kubwa alizozifanya katika kutafuta wadau mbalimbali waliosaidia kugharamia ukarabati na ujenzi wa shule hiyo, hatua iliyochangia kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu kwa wanafunzi.

Cheti hicho kilikabidhiwa na Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Mheshimiwa Albert Msando, katika hafla ya makabidhiano, ikiwa ni sehemu ya kutambua na kuthamini juhudi za viongozi wanaoshiriki kikamilifu katika kuhamasisha maendeleo ya jamii kupitia ushirikiano na wadau mbalimbali.

Nyaigesha, alitambuliwa kama mmoja wa viongozi wenye mchango muhimu katika kuunganisha nguvu za wadau na Serikali kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu. Jitihada zilizoonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi, wananchi na wadau wa maendeleo katika kuimarisha sekta ya elimu.

REGINALD MENGI
ENGLISH MEDIUM SCHOOL

Pre and Primary Government English Medium School

we can, we must, we will educate ourselves
for the prosperous future of our generation

2027 INTAKE
ADMISSIONS NOW OPEN



Why Reginald Mengi?

- Digital learning experience
- Academic excellence
- Well stocked school library
- Spacious sports grounds
- Dedicated and loving teachers
- Small classes per teacher
- Specialized reading programme
- Reliable school bus service

New Admissions: Pre-Primary and Standard One

Transfer Admissions: Standard Two, Three, Five and Six

Application Forms: Available at the school for **TZS 20,000**

Location: Sinza Madukani

Contact: 0717308980

Our fees are affordable and payable in installments.

ENROL NOW : 0717308980

SUBSCRIBE
Reginald Mengi School

Ubungo Manispaa
Dar es Salaam

@ubungomanispaa
www.ubungomc.go.tz

Shule ya msingi Msewe imeendelea kuwa chachu ya maendeleo katika eneo la Kata ya Msewe kwa kutoa fursa bora za elimu kwa watoto na kuwajengea msingi imara wa kufikia ndoto zao za baadaye. Uwepo wa miundombinu bora na ya kisasa umeongeza mvuto wa shule hiyo na kuweka mazingira rafiki yanayochochea wanafunzi kupenda kujifunza na kufanya vizuri katika masomo yao.

Aidha, shule hiyo imekuwa mfano wa kuigwa katika utoaji wa elimu jumuishi kwa kuhakikisha wanafunzi wote wanapata huduma za kielimu bila kubaguliwa kwa hali au mahitaji yao. Miundombinu iliyopo imezingatia mahitaji ya makundi mbalimbali ya wanafunzi, jambo linalosaidia kukuza usawa, ushirikishwaji na haki ya kila mtoto kupata elimu katika mazingira salama na rafiki.

Umuhimu wa shule hiyo unaonekana pia katika mchango wake kwa jamii, kwani inasaidia kupunguza changamoto za upatikanaji wa elimu bora na kuwawezesha wazazi kupata huduma za elimu zilizo karibu na maeneo yao ya makazi. Mafanikio haya yanadhihirisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya elimu ni msingi muhimu wa kujenga jamii yenye maarifa, ujuzi na uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya taifa.





Na huu, ndiyo muonekano wa darasa maalumu kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, vyoo vya kisasa vinavyozingatia mahitaji ya wanafunzi wote pamoja na matenki ya kuhifadhia maji, ikiwa ni sehemu ya miundombinu bora iliyopo katika shule hiyo inayolenga kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira salama, rafiki, jumuishi na yenye kukidhi mahitaji yao ya kujifunzia





Asante na Karibu
Msewe

Tunawashukuru wazazi na walezi kwa kuendelea kutuamini na kushirikiana nasi katika kujenga msingi bora wa elimu kwa watoto wetu. Tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu kuwaleta watoto katika Shule ya Msingi Msewe, mahali ambapo elimu bora, miundombinu ya kisasa, mazingira salama na elimu jumuishi vinapewa kipaumbele. Shule ya Msingi Msewe, ni mahali sahihi pa kuandaa kesho bora ya mtoto wako!